Kwa msaada wa kiroho na maombezi, tafuta Kanisa la kiroho la Kikristo ujitambulishe na ukasali huko kwa uaminifu ili upate kukua kiroho. Waebrania 10:24-25, 2Timotheo 3:16-17,1Petro 2:1-3, Ufunuo 3:5).

Sisi tunapatikana
TAG MWENGE CHRISTIAN CENTRE
KARIBU NA HOSPITALI YA MAMA NGOMA.
KARIBU SANA.







WASILIANA NASI!
IDARA YA WATOTO
MWENGE CHRISTIAN CENTER
MCHUNGAJI WA WATOTO :
NDG. NEEMA MUMGHAMBA
+255 713 422 233.

ROMMEDIA GOSPEL TRACTS_4423_+255 713 310 721

# WEWE NI WA THAMANI SANA MBELE ZA MUNGU !



## YESU ANATUPENDA WATOTO SISI NI WAPEKEE !

Marko 10:14b

TUNAMPENDA YESU KWAKUA ALITUCHAGUA NA ALITUPENDA KWANZA, 1 Yoh 4:19.

**Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua,
na kabla hujatoka
tumboni, nalikutakasa;
nimekuweka kuwa nabii wa mataifa**

Yer. 1:5

**Mtoto mpendwa**, Hebu angalia jambo zuri na la kushangaza sana. Hakuna mtu duniani kote ambaye yupo kama wewe. Wewe ni mtoto wa pekee sana.





Mungu ni mwenye hekima sana hivi kwamba alibuni uumbaji na mpangilio mpya kwa kila mtu. Muda mrefu kabla ya kuzaliwa alipanga jinsi utakavyoonekana, kutoka juu ya kichwa chako hadi vidole vyako. Alikujua na kukuchagua toka ukiwa tumboni mwa mama yako na kukufanya kuwa mtumishi wake kwa kusudi maalum hapa duniani, (**Yeremia.1:5).**

Mungu alikufanya wa pekee sana kwa sababu **ANAKUPENDA**. Amekuumba ili umjue, na umpende tena. (**1 Yohana 4:19).**
Kitabu maalum cha Mungu, Biblia, kinasema kwamba Mungu anajali kila ndege wa angani **(Mathayo 10:29)**. Lakini anapendezwa nawe zaidi (Mathayo 10:31)! Mungu anajua kila kitu kuhusu sisi. Anajua mambo mazuri tunayofanya na mambo mabaya ambayo hatutaki mtu yeyote ayafanye. Biblia inasema kwamba sisi sote tumefanya mambo mabaya (Dhambi) na kwamba sote tunastahili kuadhibiwa kwa kuyafanya Dhambi **(Warumi 3:23; 6:23).**

Wewe na mimi ni wa muhimu sana mbele za Mungu hivyo akaona tusipate adhabu kwa kutenda dhambi hivyo akamtuma Mwana wake wa pekee, YESU KRISTO, ili afe msalabani na kuchukua adhabu tuliyostahili.
*"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16)."*

Mungu anakupenda sana hata anataka kukusamehe dhambi zako. Lakini kwanza lazima ukubaliane naye kwamba umetenda dhambi. **(Warumi 3:23-24, Isaya. 53:6, 64:6)** Ni lazima pia uamini Yesu alikufa ili uweze kusamehewa na kuishi na Mungu mbinguni siku moja. **(Marko 16:16)** Ikiwa kweli unaamini hilo kwa moyo wako wote, sasa hivi unaweza kuzungumza na Mungu. Mwambie kwamba unakubali kifo cha Yesu ili kuchukua adhabu ya dhambi zako. Yeye yuko tayari kukusikiliza kila wakati. Anataka uwe sehemu ya familia yake na kukusaidia kila siku! Zungumza na Mungu kwa sala hii;

"Bwana Yesu, naomba unisamehe na uyafute makosa yangu yote ninayokumbuka na nisiyokumbuka; Uniokoe na dhambi zangu zote, unitakase dhambi zangu zote kwa damu yako ya thamani. Nampinga shetani ndani ya maisha yangu leo. BWANA YESU naomba unijaze Roho wako Mtakatifu ili aniongoze kwenye kweli yote na kunifundisha yanipasayo kutenda. Katika jina la YESU KRISTO AMEN.